

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI
YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) MHESHIMIWA
ANGELLAH J. KAIRUKI (MB) KWENYE UFUNGUZI WA
MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
TAREHE 06/04/2017**

*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa OR-Menejimenti ya
Utumishi wa umma na Utawala Bora,
Naibu Katibu Mkuu,
Mwenyekiti wa TUGHE – Taifa,
Katibu wa TUGHE – Taifa,
Wajumbe wa Baraza,
Wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana,*

1. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe na Uongozi wa Baraza katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kunishirikisha kuja kufungua mkutano huu muhimu, Asanteni sana.

Aidha, nawapongeza wajumbe na washiriki wote kwa kuhudhuria na kushiriki kwenye Baraza hili muhimu, katika jitihada za kuimarisha utendaji kazi na ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kujadili masuala muhimu ya Utumishi wa Umma. Pia, niwapongeze waandaaji wa Mkutano huu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Vilevile napenda niwashukuru wageni

waalikwa toka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) ngazi ya Taifa, Mkoa na Tawi na Mwakilishi toka Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), kwa kuitikia mwaliko wa kushiriki katika kikao hiki leo. Naamini kuwepo kwenu hapa kutakuwa ni chachu ya mawazo katika majadiliano ambayo yatasaidia kuimarisha hali za watumishi na utendaji kazi katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

2. Mwenyekiti na wajumbe, lengo la kuwa na Baraza la Wafanyakazi ni kutoa fursa kwa Watumishi, kupitia wawakilishi wao, kujadiliana juu ya masuala mbalimbali ya msingi yanayohusu tija na ufanisi kwa upande mmoja na kwa upande mwingine maslahi yao kama Watumishi. Hili ni jambo jema, kwa sababu ni utaratibu unaoimarisha ushiriki wa kweli wa wafanyakazi katika uendeshaji wa Ofisi. Hivyo basi, kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza katika mikutano yangu mbalimbali ninapokutana na Viongozi, Watumishi wa Umma au wawakilishi wao, ni vyema tuchukue pia fursa hii kujadiliana na kutafakari, si maslahi yetu tu bali pia, utendaji wetu wa kazi wa kila siku na jinsi ya kuuboresha zaidi. Hii ni kwa sababu tija na maslahi ni matokeo ya utendaji bora, unaolenga kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wa Tanzania. Aidha, Tija ndio chimbuko la maslahi bora kwa Watumishi na msingi wa mkakati wa kukuza uchumi nchini.

